**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA DODOMA, DR. BINILITH S. MAHENGEWAKATI WAUFUNGUZI WA KONGAMANO LA UWEKEZAJI MKOA WA DODOMA TAREHE 27 JUNI, 2019**

Mhe. Kasim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Job Ndugai (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Waheshimiwa Mawaziri,

Waheshimiwa mabalozi,

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa,

Ndugu, Makatibu Wakuu wa Wizara,

Ndugu, Makatibu Tawala wa Mikoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma,

Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya

Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Serikali,

Wakurugenzi wa Halmashauri,

Wawekezaji mbalimbali mlio hapa,

Waandishi wa Habari,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na uzima aliyotujalia sisi sote, kujumuika pamoja mchana huu wa leo kwenye tukio hili la kihistoria la kuzindua Kongamano la Uwekezaji kwa mara ya kwanza baada ya Serikali kuhamishia Makao yake Makuu Mkoani Dodoma. Sisi Wananchi wa Mkoa wa Dodoma tunafuraha isiyo kifani kwa heshima uliyotupatia ya kukubali kuwa Mgeni rasmi wa tukio hili. ***Tunasema ahsante sana kwa heshima hii kubw***a. Aidha napenda kutumia fursa hii kuwakaribisha viongozi,wawekezaji na wageni  wote hapa katika jiji la Dodoma na mjisikie mpo nyumbani. ***Karibuni sana***

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Katika kufikia azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, Mkoa wa Dodoma umeandaa Kongamano hili la uwekezaji kwa lengo la kutangaza fursa na vivutio vya Uwekezaji vilivyopo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma ili kuvutia uwekezaji wa Ndani na Nje ya Nchi. Kauli Mbiu yake ni ***‘Dodoma Fursa Mpya ya Kiuchumi Tanzania, Wekeza Dodoma, Tukufanikishe***’ Kauli mbiu

hii inatanabahisha nafasi ya Mkoa wa Dodoma kwa sasa na mbeleni katika mustakabali wa Uchumi na Utawala wa Nchi. Aidha, inatoa tamko la azimio la uongozi na kujenga imani ya utayari wa Mkoa wa Dodoma katika kujenga Mazingira Wezeshi kwa wawekezaji kwamba Wekeza Tukufanikishe.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Mkoa wa Dodoma unazo sifa kadhaa zinazoufanya uvutie kwa uwekezaji kama ifuatavyo;

- **Kuwa makao makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. *Fursa kubwa ya uwepo wa soko la bidhaa mbalimbali zitakazozalishwa hapa na soko kubwa la mahitaji ya huduma za jamii kutokana Idadi kubwa ya watu wanaohamia Dodoma wenye kipato cha Kati na Kikubwa,Wageni kutoka mataifa mbalimbali,mabalozi na Taasisi za kimataifa.Fursa nyingi za uwekezaji na biashara kwenye ujenzi wa Makao Makuu Mapya ya Nchi katika karne ya 21 ya sayansi na teknolojia za kisasa.*
  *Wawekezaji na wafanyabiashara hawahitaji kufanya utafiti wowote ili kuwekeza/kufanya biashara kwasababu ni wazi kwamba Dodoma ,Kama makao makuu ya NCHI mahitaji ya hotel za kisasa,nyumba za wageni,huduma za afya za kisasa na shule za kimataifa nk hayakwepeki.****Napenda kwa Niaba ya***

***Serikali Mkoa na wananchi kutoa pongezi na shukurani kwa Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli kwa uamuzi wake thabiti wa kuhamishia makao makuu ya serikali Mkoani Dodoma ambacho ndio kichocheo na chanzo kikuu cha fursa nyingi za uwekezaji.***

- Uwepo wa ardhi iliyotengwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwekezaji. Jumla ya Hekta 12,090 zimetengwa na Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya uwekezaji katika Nyanja mbalimbali kama kilimo, viwanda, taasisi (elimu, afya), uendelezaji miliki (Makazi, hoteli na Majengo ya biashara (Commercial Building).

- Ili kurahisisha na kufanikisha mazingira ya uwekezaji Dodoma, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimefungua ofisi ya Kanda ya Kati ambayo ofisi zake zipo Dodoma. Huduma mbalimbali zikiwepo kupata taarifa na taratibu za uwekezaji, maombi ya vibali na leseni mbalimbali za uwekezaji kwa wawekezaji wanaowekeza Dodoma zinaratibiwa na ofisi hii. Wawekezaji wa ndani na nje wamechangamkia fursa hii ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Juni 2019, jumla ya miradi mipya 22 imesajiliwa katika Mkoa wa Dodoma ambayo inatarajia kuwekeza mtaji wa Dola za Marekani 232.51 Milioni na kuzalisha ajira mpya 2,867.

- Urahisi wa kufikika kutokana na kuwa katikati ya Nchi.
- Mkoa wa Dodoma umeunganishwa na miundombinu ya usafiri na usafirishaji mizuri (Barabara za lami zinazounganisha na mikoa mingine na kiwanja cha ndege).Ujenzi wa miundombinu ya usafifirishaji unoendelea sasa: SGR,Barabara za pete ya ndani na nje,Uwanja wa kimataifa wa ndege Msalato,Stendi ya kisasa na soko
- Mawasiliano yameendelea kuimarishwa. Mitandao ya simu ipo hadi vijijini. Ongezeko la watu linavutia uwekezaji.
- Usambazaji wa umeme umeenea hadi katika maeneo ya Vijijini. Hivi sasa vijiji 304 katika Mkoa wa Dodoma vimesambaziwa umeme kupitia mradi wa REA kati ya 593 sawa na asilimia 51. Uzalishaji wa umeme ni MW 48 wakati matumizi ni MW 28. Kwa hiyo kwa sasa matumizi ni chini ya uzalishaji uliopo.Tanesco wanaendelea na kujenga miundombinu ya kuongeza uzalishaji umeme.Mradi mkubwa wa uzalishaji umeme wa Stiller's gauge
- Usambazaji wa maji unaendelea kuimarishwa. Takriban asilimia 80 ya wakazi wa Jiji la Dodoma wamefikishiwa maji. Kwa sasa DUWASA ina uwezo wa kuzalisha lita milioni 61.5 kwa siku. Hivi sasa DUWASA inazalisha lita million 52 kwa siku ambazo zinakidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa. DUWASA

itaendelea kuongeza kiasi cha uzalishaji kwa kadri Miundombinu ya usambazaji itakavyoendelea kuongezwa. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa ujenzi wa bwawa kubwa la Maji katika Kijiji cha Farkwa Wilayani Chemba ambalo linatarajiwa kuwa chanzo cha uhakika cha maji kwa mji wa Dodoma na Vijiji vitakavyopitiwa na mradi huo.

- Uwepo wa Usalama na amani:

  Hali ya hewa nzuri: Tofauti za joto la Mchana na usiku zinaifanya Dodoma maghala pazuri pakufanya Kazi ofisini nyakati za mchana na mahala pazuri pa kulala nyakati za usiku bila matumizi ya viyoyozi***.***

  ***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na fursa nyingi zinazovutia uwekezaji katika Mnyororo wa thamani kama ifuatavyo;

**Kwanza,** Fursa zinazotokana na Serikali kuhamishia makao makuu katika Mkoa wa Dodoma. Kasi ya ongezeko la watu wenye kipato cha kati na cha juu ni fursa inayoifanya Dodoma kuvutia uwekezaji katika;

- Ujenzi wa nyumba za Biashara (Shoping malls)
- Ujenzi wa mahoteli ya hadhi ya nyota tano n.k
- Ujenzi wa nyumba za makazi

- Hifadhi ya bidhaaa za usambazaji wa bidhaa kwenda maeneo mbalimbali
- Usafirishaji wa mizigo
- Usafirishaji wa abiria ndani ya Jiji
- Kuendeleza shule na vyuo vya hadhi ya kimataifa
- Kuendeleza huduma za tiba na afya za kibingwa
- Uendelezaji wa maeneo huru ya biashara

**Pili,** Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na hali ya hewa inayofaa kuzalisha mazao ya kilimo. Pamoja na mazao mengine ipo fursa katika uzalishaji wa mazao ya kimkakati ambayo ni zabibu, mihogo, Mtama na mazao ya mbegu za mafuta (alizeti, Karanga, ufuta na Pamba).

Hivyo, Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika maeneo yafuatayo;

- Uzalishaji wa mazao hayo kukidhi mahitaji ya viwanda vilivyopo na vitakavyoanzishwa
- **Viwanda vya kusindika** zao la alizeti na zabibu vyenye teknolojia bora ili kuzalisha bidhaa zinazokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.
- **Kwa zao la zabibu tunahitaji viwanda** zaidi vitakavyozalisha bidhaa mbalimbali kama mchuzi,mvinyo, juice na zabibu za kukausha**.**

- **Viwanda vya kutengeneza vifungashio**. Wapo wajasiriamali wengi wa vyakula kama unga, siagi, asali ambao wamekuwa wakilalamika ukosefu wa vifungashio vyenye ubora unaokidhi viwango.
- **Kilimo cha Mkataba na wanunuzi wakubwa wa Mazao**. Dodoma inao wakulima wadogo wachapakazi waliotayari kuzalisha mazao mbali.
- **Kilimo cha umwagiliaji** kwa kutumia fursa ya kuvuna maji ya mvua na maji chini ya ardhi
- **Utengenezaji wa vifungashio** hasa kwa wasindikaji wadogo wa vyakula, asaliPamoja na nyongeza ya fursa kubwa inayotokana na ujio wa Makao Makuu ya Serikali, Mkoa wa Dodoma una rasilimali nyingi mahsusi ikiwa ni pamoja na ardhi inayofaa kwa uzalishaji katika kilimo na ufugaji na mandhari nzuri kwa utalii.
- Mawakala wakubwa wa pembejeo za kilimo

**Tatu,** Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na hali ya hewa inayoruhusu mifugo ya aina mbalimbali hususan Ng'ombe, mbuzi, Kondoo na kuku. Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika;

- Uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama
- Uzalishaji wa malisho ya mifugo
- Usindikaji wa vyakula vya mifugo

- Uchakataji wa ngozi na bidhaa zitokanazo na ngozi
- Uzalishaji wa mayai
- Usindikaji wa nyama ya ngome, mbuzi, Kondoo na maziwa
- Huduma za afya ya mifugo
- Mawakala wa pembejeo za mifugo

**Nne,** Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na madini ya aina mbalimbali kama dhahabu,vitona madini ya ujenzi. Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika;

- Uchimbaji Mkubwa wa madini hususan dhahabu na vito.
- Ununuzi wa madini kutoka kwa wachimbaji wadogo
- Uongezaji wa thamani wa madini zinazozalishwa dhahabu na vito.

**Tano,** Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na vivutio mbalimbali vya utalii. Yapo Mapori ya Wanyamapori ya Swagaswaga na Mkungunero na Sehemu kubwa ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangine ipo Dodoma. Aidha, Mkoa wa Dodoma umeunganishwa vizuri kwa barabara za lami kwenda kwenye Hifadhi za Taifa za Manyara, Ngorongoro na Ruaha. Kwa upande wa mbuga ya Ruaha lipo lango la kuingilia hifadhini katika Kijiji cha Mpwayungu Halmashauri ya Chamwino ambapo ni Kilomita 120 tu kutoka hapa Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu,**

Vipo vivutio vingine kama maeneo ya Kihistoria yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa Nchi zilizo kusini mwa Afrika, Michoro ya miambani na utalii wa kitamaduni. Hivyo, wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika;

- Hoteli za Kitalii
- Nyumba za wageni
- Makampuni ya utalii (Tour operators)
- Kuendeleza utalii wa kitamaduni

**Sita,** Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na misitu vinavyofaa kwa ajili ya uzalishaji wa asali. Tunakaribisha uwekezaji katika;

- Uzalishaji wa asali
- Uchakataji wa asali
- Uzalishaji wa nta na bidhaa zinazozalishwa kwa nta

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Mkoa wa Dodoma katika ngazi zake mbalimbali, unawahakikishia wawekezaji kuwa:-

- Watapata Ulinzi na Usalama wa kutosha
- Watapata ardhi kwa ajili ya uwekezaji bila kuchelewa
- Upatikanaji wa miundombinu na mifumo rafiki

- Usaidizi na uwezeshaji wa kitaalam katika uzalishaji na biashara

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Matarajio ya Mkoa wa Dodoma katika siku hizi mbili ni:-

- Kuzitangaza fursa za uwekezaji na biashara zilizopo katika Mkoa wa Dodoma
- Kukutanisha wawekezaji wa mitazamo ya aina moja na tofauti kwa ajili ya kujadiliana na kujenga ubia
- Kufanya majadiliano ya kisekta (B to B) ili kuwianisha minyororo ya thamani
- Kufahamiana na viongozi wa ngazi zote katika Mkoa
- Kusaini MoU kwa wawekezaji watakao kuwa tayari kuweka kuweza,taratibu zote zimeandaliwa hasa ukizingatia kwamba ofisi zote za serikali zipo hapa Dodoma.

**SHUKURANI**

- ***Chama cha Mapinduzi***; Kwa kuruhusu Kongamano hili kufanyika katika ukumbi huu na kwa Miongozo thabiti kupitia Ilani yake ya Uchaguzi;
- ***Waziri wa Nchi OFISI ya WM***:Natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Angela Kairuki (Mb) , Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji kwa juhudi zake anazofanya katika

kukuza uwekezaji nchini na hususan katika kufanikisha Kongamano la Uwekezaji hapa Dodoma.

• ***Kamati ya Maandalizi***: Napenda kuishukuru sana kamati ya maandalizi iliyo ongozwa na katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Maduka Kessy, Wataalam ngazi ya Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Mabaraza yote ya Halmashauri zote nane za Mkoa wa Dodoma na Wajumbe kutoka Sekta Binafsi: Prof Mlacha, Ringo Iringo Kofia na Iddi Mungwe;

• ***Wadhamini wa Kongama***no; UNDP, LIC, Halmashauri ya Jiji, Benki za CRDB, NMB na TIB - Develoment, TCRA, TANAPA, TIC, PSSSF, BRELA na Daudi Msungu kwa kufadhili maandalizi ya Kongamano hili;

• ***ESRF (Economic and Social Reseach Foundation) kwa maandalizi ya Kitabu cha Andiko la Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji Mkoa wa Dodoma (Dodoma Region Investment Guide);***

• ***Makampuni/sekta binafsi***: Kampuni za S&Y, DALBERG CETAWICO, Nyanza Construction Works, CRJE, Direct Agency, Magodoro Dodoma, na ALKO VINTAGE, Geoplan Limited, Land network, Chuo Kikuu St Johns, Mngwabi na Wendeche na Ringo Iringo Kofia kwa kuchangia kufanikisha Kongamano hili;

• ***Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma kwa kufanikisha maandalizi ya Kongamano hili***

- Mashirika ya Umma: TAWA, TBS, Watumishi Housing, TANTRADE, NHIF, Wizara ya Viwanda na Biashara, Geological survey of Tanzania
- Chemba ya Wafanyabiashara, wenyeviwanda, Wakulima (TCCIA) na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) kwa kuchangangia, kushiriki maandalizi na kuwa sehemu ya Kongamano.
- ***Kampuni ya Home of Event***s: Kwa kuratibu Maandalizi ya Kongamano hili na kulifanya kuwa na sura mnayoiona. Tunawapongeza sana kwa ushirikiano mliotuonyesha.
- ***Waheshimiwa Mabaloz***i wa Nchi mbalimbali hususan; Ufaransa, Uholanzi, Uganda, Namibia, Zimbabwe, Nigeria, Msumbiji na Burundi kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya awamu ya Tano na kushiriki Kongamano hili.
- ***Waliotuchangia: Kwa kujisajili na kuchangia gharama za Kongamano***
- ***Washiriki***: Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi na Idara za kiserikali, Wakuu wa Makampuni binafsi, Wafanyabiashara na Wawekezaji binafsi;
- ***Watoa huduma mbalimbali;***

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Nihitimishe kwa Kukushukuru tena kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Kongamano hili na nichukue fursa hii kuwakibisha tena wadau wote waliohudhuria Kongamano hili. Tunaahidi kushirikiana kwa karibu na kuwawezesha wawekezaji wote kufanikisha uwekezaji wao hapa Dodoma.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Sasa naomba nichukue fursa hii kumkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji Mheshimiwa Angela Kairuki atoe salaam za Wizara na akukaribishe kuongea na hadhara hii.

Nashukuru sana Mheshimiwa Rais

***Asanteni kwa kunisikiliza***